# HOTUBA YA MGENI RASMI

## MKUU WA WILAYA YA TANGA KWENYE UFUNGUZI WA WARSHA YA KUKUZA BIASHARA KWA WAJASIRIAMALI WA TANGA

18/04/2024 Ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga.



Download Viwango App on
GET IT ON Google Play
Download on the App Store

# HOTUBA YA MGENI RASMI MKUU WA WILAYA YA TANGA KWENYE UFUNGUZI WA WARSHA YA KUKUZA BIASHARA KWA WAJASIRIAMALI WA TANGA, INAYO FANYIKA LEO TAREHE 18/04/2024 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA.

1. MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA,
2. MENEJA WA SIDO MKOA WA TANGA,
3. AFISA MTENDAJI MKUU (CEO) WA SCANCODE,
4. MKURUGENZI MTENDAJI WA KAMPUNI YA ANJARI - MDHAMINI MKUU WA AWARSHA HII)
5. WAWAKILISHI WA TAASISI ZITAKAZO TOA MAFUNZO (SIDO, TRA, TBS, BRELA, GCLA, UTT Amis & SCANCODE YENYEWE),
6. WAJASIRIAMALI WETU MTAKAO SHIRIKI MAFUNZO,
7. WANAHABARI,
8. WAGENI WAALIKWA, Mabibi & Mabwana,

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.........**
**Kazi iendeleee.............**

**Awali ya yote,**
Nami nianze kwa kumshukuru Muumba wetu kwa Rehema zake kwa kutujalia Uhai, Afya na Nguvu za kuwepo hapa siku ya leo,

**Pili,**

Ninakushukuru wewe Afisa Mtendaji Mkuu (CEO) wa SCANCODE TANZANIA pamoja na timu yako yote, kwa ujasiri na ubunifu mkubwa kwa kuweza kuwa wazalendo wa Taifa Letu na kuanzisha kamapuni hii muhimu kabisa, ambapo kimsingi ni taasisi muhimu sana kwa wakati wa sasa katika kujibu changamoto nyingi za kiteknolojia kwa wajasiriamali wetu. Hivyo kwa niaba ya Serikali, nawapongeza sana kwa moyo huo wa dhati wa kukusudia kuwasaidia wajasiriamali wetu ili waweze kuinuka kiuchumi na kulisaidia Taifa letu.

**Tatu,**

Nilipongeza sana Shirika letu la kuendeleza Viwanda vidogo hapa nchini yaani SIDO kwa uamuzi sahihi wa kujenga mahusiano ya kikazi ya kushirikiana na SCANCODE ili kwa pamoja mtoe elimu ya jinsi ya kuwasaidia wajasiriamali wetu kuweza kunufaika na kazi zao na pia kusaidia kukuza zaidi nguvu kazi yenye ujuzi wa kileo ambapo sasa wajasiriamali wetu kupitia SIDO watajua na kunufaika na teknolojia ya mawasilianao ya habari kwa kuwezesha kupata alama muhimu kabisa za Barcodes na QR Codes kutoka SCANCODE.

Aidha, Shirika la SIDO ndio kitovu cha kukuza na kuendeleza nguvu kazi ya Taifa na kusaidia kuongeza ujuzi na utaalamu kwa wajasiriamali wetu, tena husasani kwenye upande wa teknolojia jambo ambalo ni muhimu sana kwa ufanyaji biasahara wakati wa sasa.
Pia nampongeza sana Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga kwa kuridhia kutumia ukumbi huu kwa ajili ya shughuli yetu hii ya leo.

## Nne:

Nawapongeaza sana wajasiriamali wote mliojitokeza kushiriki kwenye mafunzo haya. Mmeona umuhimu na manufaa ya kuzijua na kuzitumia huduma za SCANCODE katika kuendeleza biasahara zenu. Jifunzeni warsha hii kwa kusikiliza kwa makini mafunzo haya kutoka kwa wataalamu wetu taasisi zilizo andaliwa kufundisha, ili mjue mbinu za kuwasaidia kupata fursa pana zaidi za masoko ya bidhaa mtakazo zizalisha.

Ni kweli suala la kujisajili kupata Barcodes kwenye bidhaa za wajasiriamali hapa nchini kwa muda mrefu lilikuwa ni chanagamoto kubwa kwani, uwezo wa kimtaji wa wengi wenu kumudu gharama zake ilikuwa ngumu. Lakini leo tumesikia SCANCODE imekuja na majibu ya kuwasaidia.

Mtaweza kusajiliwa kupata sio tuu Barcode peke bali pia na alama za QR Code ambazo ndio ufunguo wa kujitambulisha kwenye bidhaa na huduma kwa sasa ulimwenguni. Hakuna gharama ya kujisajili yaani Registration Fees, huu ni mchango mkubwa sana kutoka kwa kampuni ya SCANCODE TANZANIA.

Ni wito wangu kwa wajasiriamali wote wa Tanga mtazitumia vyema huduma hizi ili mnufaike mara dufu kwenye ujasiriamali wenu. Mlio bahatika kuanza kwenye hii warsha ya awamu ya kwanza, nendeni mkawe pia mabalozi kwa wengi ili kesho na kesho kutwa SIDO iweze tena kuandaa warsha nyingine kuwanufaisha wajasiriamali wote.

## Tano:

Naipongeaza kwa Dhati kampuni yetu ya hapa Jijini Tanga ya M/s ANJARI kwa uzalendo wao wa kudhamini sehemu ya gharama za warsha hii. Ni wazi kabisa mmeamua kurejesha kwa jamii sehemu ya faida mnayoipata kwenye biasahara zenu na kufadhili mafunzo haya ya wajasiriamali. Hongera sana Mkurugenzi Mtendaji wa ANJARI Soda Factory Ltd Katika hili, naomba nitoe wito kwa makampuni mengine ya Jijini Tanga kuiga mfano huu wa kamapuni ya ANJARI katika kuiunga mkono serikali katika kudhamini mafunzo kwa wajasiriamali. Huu ni mfano nzuri wa kuigwa hivyo naipongeza sana kampuni ya ANJARI kwa moyo wa kizalendo.

## MPANGO WA SERIKALI KATIKA KUWAINUA WAJASIRIAMALI.

Serikali ya Awamu ya Sita inayo ongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan ina malengo mahususi kabisa ya kusaidia makundi mbalimbali ya jamii yakiwemo ya wajasiriamali wanawake, vijana na makundi maalumu kwa kutenga asiliami 10 ya mapato ya ndani ya kila Halmshauri ili zisaidie kupata mitaji ya kuendeleza na kuwezesha shughuli za ujasiriamali nchini.

Aidha, ni matokeo ya sera madhubuti za Chama cha Mapinduzi katika kusaidia wananchi wake kujikwamua kiuchumi. Hivyo wananchi wote kwenye maeneo yetu ni lazima kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais wetu Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kufanya kazi kwa bidii zaidi na kwa ubunifu zaidi kulingana na mazingira ya sasa ya matumizi ya teknolojia.

SCANCODE kwa kushirikiana na SIDO wameonesha njia ya jinsi ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan katika kuukwamua uchumi, hivyo ili kuonesha kujali, kuheshimu na hata kuthamini juhudi za Mheshimiwa Rais Dkt Samia, basi tutumie kila fursa serikali inayo iandaa na kuileta kwenu ili mnufaike na kuujenga zaidi uchumi wa mtu mmoja mmoja lakini pia kwa Taifa zima kwa ujumla.

## KUHUSU OMBI LA KUITANGAZA ZAIDI HUDUMA YA SCANCODE.

### Ndugu Afisa Mtendaji Mkuu wa SCANCODE,

Ombi hili halikupaswa kuwa ombi kwa sisi viongozi na watendaji wa Serikali. Bali kuisemea kwa umma ili huduma za SCANCODE zitambulike kwa kila mjasiriamali ni jukumu la kila kiongozi au mtendaji serikalini. SCANCODE huduma zake zikienea nchi nzima, na kila mtu akajua manufaa ya kutumia huduma za Barccodes na QR Code kwenye bidhaa zinazo zalishwa nchini, kutapaisha juu zaidi uchumi wetu wa Tanzania kwani ndilo lengo la serikali ya CCM kuufanya uchumi wa Tanzania uimarike zaidi na zaidi.

## RAI KWA TAASISI ZOTE ZA KIBIASHARA ZINAZO WALEA WAJASIRIAMALI.

Shirikianeni kwa pamoja katika kuwezesha huduma za SCANCODE zijulikane vyema kwa wajasiriamali wetu. Pia kwa mabaraza yetu ya Madiwani kwa maana ya upande wa Serikali za Mitaa (LGA), maafisa Biashara na maafisa Maendeleo ya Jamii himizeni wajasiriamali kutumia huduma hizi za kisasa katika kuwasiliana ili kusaidia kutanua zaidi wigo wa masoko ya ndani na nje ya nchini. Ikiwezekana madiwani wetu waangalie jinsi ya kuunda sheria ndogo ndogo za kuhimiza matumizi ya Barcodes na QR Code kwenye bidhaa na pasiwepo na mjasiriamali yeyote atakae shindwa kuweka alama hizo kwenye bidhaa yake kwa vile tuu sasa hakuna gharama za kujisajili na SCANCODE kupitia ofisi za SIDO wapo muda wote kuwasaidia.

## HITIMISHO,

Nirudie tena kuipongeza SCANCODE TANZANIA na SIDO kwa kuandaa warsha hii muhimu sana.
Fanyeni jambo hili kwa moyo kabisa huku mkijua serikali ipo nyuma yenu kuwaunga mkono.
Nitafurahi pia mkituletea mrejesho ofisini kuhusu ni wangapi wamepatiwa mafunzo haya na wako wapi na je, matarajio yao baada ya mafunzo haya ni yapi ili sisi kama Serikali tuweze kuwapatia pia taarifa watunga sera na mipango mbalimbali ya kuendeleza shughuli za uchumi na biashara, mikakati yetu ili maboresho yafanyike zaidi kuwanufaisha wajasiriamali.

***Kwa kusema hayo, natamka rasmi kuizindua warsha hii ya kukuza na kuendeleza biashara za wajasiriamali hapa jijini Tanga leo April 18, 2024.***

# *AHSANTENI SANA.*

## Contacts:

**For more infomation please use the following contacts:**


COSTECH Building, Ali Hassan Mwinyi Rd
Kijitonyama, Dar es salaam

+255 716 441 084
+255 743 437 867,
info@scancode.co.tz
www.scancode.co.tz